Nia Iliyofanywa Upya (The Renewed Mind)

Na

Ellis P. Forsman

Nia Iliyofanywa Upya

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Nia Iliyofanywa Upya

Rum. 12:1-21

Maisha ya Ukristo yanapaswa kuwa maisha yenye mabadiliko…

Maisha yasiyofuatisha vitu vilivyoko katika dunia hii.

Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"

Maisha ya Ukristo pia hutafuta kuthibitisha (kuonyesha) kwamba njia ya Mungu ni bora.

Maisha ya Ukristo inahitaji kuzifanya upya nia zetu itakayofanya tujifunze mapenzi ya Mungu; na kuweza kufanya iwezekane kugeuzwa.

Ni ishara zipi zinaonyesha nia iliyofanywa upya? Katika Rum. 12:16 tunapata nia au mtazamo unaopatikana miongoni mwa Wakristo.

Rum. 12:16, "*Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, lakini mkubali kushughulishwa na mambo manyonge. Msiwe watu wa kujivunia akili.*"

Angalia kwanza kwamba kunapaswa kuwa na…

Kupatana kwa nia

Hii inamanisha…

Biblia ya NKJV inasomeka, "Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi…"

Kiuhalisia, "fikiria jambo ilo hilo".

Himizo ambalo wakati wote Wakristo wanahimizwa:

Wakristo katika Rumi.

Rum. 15:5, "Na Mungu mwenye saburi na faraja awajalie kunia mamoja ninyi kwa ninyi, kwa mfano wa Kristo Yesu."

Wakristo katika Korintho.

1 Kor. 1:10, "*Basi ndugu nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*"

Wakristo katika Filipi kwa wakati ule walikuwa na tatizo katika umoja.

- Fil. 1:27, "*Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikiee mambo yenu kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili.*"
- Fil. 2:2-3, "*Ijazilizeni furaha yangu ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja. Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake.*"
- Fil. 3:16, "*Lakini, hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo.*"
- Fil. 4:2, "*Namsihi Euodia, namsihi na Sintike, wawe na nia moja katika Bwana.*"

Wakristo kule Asia.

1 Pet. 3:8, "*Neno la mwisho ni hili, mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitivu, wanyenyekevu;*"

Kama Wakristo wanavyofanywa upya nia zao wataanza kuwa na malengo yanayofanana, kusudi, mitazamo, nk.

Tunaambiwa kuja pamoja na kusemezana.

Isa. 1:18, "*Haya, njooni tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*"

Hii inawezekanaje...

Mara nyingi watu wanajaribu kusemezana bila Bwana

Tunapaswa kutafuta nia ya Kristo.

Fil. 2:5, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwa pia ndani ya Kristo Yesu;"

Kila mtu anapaswa kujitahidi kujenga na kutazama nia ya Kristo.

Kadiri tunavyokuwa kama yeye, ndivyo tunavyokuwa karibu naye "*wa nia ile ile.*"

Tunaweza kuwa na nia ileile kwa kuelekeza nia zetu katika vitu vilivyoko juu.

Kol. 3:1-2, "*Hatimaye ndugu zangu furahini katika Bwana. kuwaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi. Jihadharini na mbwa, jihadharini na matendo maabaya, jihadharini na wajikatao.*"

Kiloa mmoja anapaswa kuweka mitazamo yao katika mambo ya kiroho.

Amechanganywa na mambo ya dunia na mitazamo ya kibinadamu, umoja wa nia utaangamizwa.

Hatuwezi kupata nia ya Kristo kupitia mitazamo yawanadamu.

Pale ambapo hakuna umoja, mtu (labda kila mtu) hawaweki nia zao kwa Kristo na vitu vilivyoko juu!

Tunaporudi katika kifungu chetu (Rum. 1:2, 16), tunapata kwamba mwonekano mwingine wa "*Nia iliyofanywa upya*" ni…

Nia inayojishusha

Hii inamanisha nini.

"*Msinie yaliyo makuu.*" (NKJV).

Paulo analizungumzia hili kwenye barua yake kwa Wafilipi:

Fil. 2:3, "*Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenzake kuwa bora kuliko nafsi yake.*"

"Usiwe vutane."

"Usiwe mgomvi."

"*…bali shirikiana na wanyenyekevu.*" (NKJV).

"Shirikiana na wapole."

"Changamana na watu wa kawaida."

Nia iliofanywa upya hufanya juhudi za msingi ili kusiwe na maajivuno, na inapenda kushirikiana na watu wenye shughuli za kawaida na wapole.

Hii inawezekanaje…

Kwa kushikilia kile tunachojifunza:

Mtazamo wa Daudi.

Zab.131:1-2, "*BWANA moyo wangu hauna kiburi, wala macho yangu hayainuki. Wala sijishughulishi na mambo makuu, wala na mambo yashindayo nguvu zangu. Hakika nimeituliza nafsi yangu, na kuinyamazisha. Kama mtoto aliyeachishwa kifuani mwa mama yake; kama mtoto aliyeachishwa, ndivyo roho yangu ilivyo kwangu.*"

Onyo la Yeremia.

Yer. 45:5, "*Je unajitafutia mambo makuu? Usiyatafute kwa maana tazama, nitaleta mabaya juu ya wote wenye mwili, asema BWANA; lakini roho yako nitakupa iwe nyara, katika mahali pote utakapokwenda.*"

Fundisho la Yesu.

Luka 22:24-27, "*Yakatokea mashindano kati yao kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa. Akawaambia wafalme wa wa mataifa huwatawala, na wenye mamlaka juu yao huitwa wenye fadhili; lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye. Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani, au yule atumikaye? Siye yule aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye.*"

Kwa kuzingatia kile tunachojifunza:

Mfano wa Yesu.

Fil. 2:5-8, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu chaa kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya utumwa, akawa ana mfano waa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadaamu alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*"

Fundisho la Yakobo.

Yak. 2:1-5, "*Ndugu zangu imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, msiwe nayo kwa kupendelea watu. Maana akiingia katika sinagogi lenu mtu mwenye pete ya dhahabu na mavazi mazuri; kisha akiingia na maskini, mwenye mavazi mabovu; nanyi mkimstahi yule aliyevaa mavazi mazuri na kumwambia, keti wewe hapa mahali pazuri, na kumwambia yule maskini, simama wwewe pale, au keti miguuni pangu, je hakufanya hitilafu mioyoni mwenu, mkawa waamzi wenye*

mawazo mabovu? Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Je! Mungu hakuwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao?"

Mtu anapokuwa na nia ya Kristo, upole wa nia yake itaonekana kwa uasili wa malengo yake na wale aanaoshirikiana nao.

Mwisho, inayofanana na upole wa nia, "Nia Iliyofanywa Upya" pia inakaa…

Upole wa nia

Hii inamanisha…

"*Usijivunie yaliyo yako mwenyewe.*" (NKJV).

"Usifikirie yaliyomakuu."

"Usiringe."

"Usifikiri kwamba unafahamu yote."

Onyo kama hilo linapatikana sehemu nyingine:

Ikitolewa na Sulemani.

- Mit. 3:7, "*Usiwe mwenye hekima machoni pako; mche BWANA ukajiepushe na uovu.*"
- Mit. 26:12, "*Je wamwona mtu mwenye hekima machoni pake mwenyewe? Afadhali kumtumaini mpumbavu kuliko yeye.*"

Imeliliwa na Isaya.

Isa. 5:21, "*Ole wao walio wenye hekima katika macho yao wenyewe, na wenye busara katika fikira zao wenyewe!*"

Paulo ametahadharisha.

1 Kor. 3:18, "*Mtu asijidanganye mwenyewe; kama mtu akijiona kuwa mwenye hekima miongoni mwenu katika dunia hii, na awe mpumbavu, ili apate kuwa mwenye hekima.*"

Nia iliyofanywa upya itakuwa na hali thabiti ya uvumilivu, kujitambua kwamba mtu ana mengi ya kujifunza kwa Mungu na wengine.

Hii inawezekanaje…

Bila shaka, kwa kuyassikiliza maandiko.

Kama hii inayopatikana katika:

1 Kor. 8:2, "*mtu akidhani ya kuwa anajua neno, hajui neno lolote bado, kama impasavyo kujua.*"

Hekima ya ulimwengu huu ni upuuzi kwa Mungu.

1 Kor. 1:20, "*Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu?*"

Mtazamo wa Napoleon. Alipanga kuikabili Urusi na kuishinda Czar. Mtu akasema mbele macho yake, "Mwanadamu anapendekeza, lakini Mungu hamiliki." Kwa kusikia kauli hii, Napoleon alijibu, "Ninapendekeza, na Similiki." Kimsingi alimwacha Mungu, na ilidhihirisha hatari. Maana Mungu alimshughulikia Naoleon kupitia moja ya kiumbe chake kidogo na ambacho hakikuwa na uwezo – kipande cha theluji. Jeshi lake halikujiandaa kwa ajili ya theluji ya Urusi, na alishindwa. "Urusi itakuwa yangu," moyo wake wa majivuno ilisema, lakini Mungu alikuwa pale.

Werevu wengi hawaipokei injili.

1 Kor. 1:26, "*Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa;*"

Huko Florida, mtu asiyeamini kwamba Mungu yupo alikasirishwa na maandalizi ya sikuu yaa Pasaka. Aliamua kuwasiliana na wakili wake kuhusu ukiritimba waliofanyiwa watu wasioamini kwamba Mungu yupo kwa sherehe zilizofanywa na Wakristo na Wayahudi kwa sikukuu zao zote wakati wasioamini kwamba Mungu yupo hawakuwa na sikukuu ya kusheherekea. Swala hili lilipelekwa mbele ya hakimu. Baada ya kusikiliza uwasilishi uliovutia na wakili, hakimu alipiga meza yaake na kutangaza, "Kesi imeahirishwa!" Mara wakili akasimama na kupinga mwongozo na kusema, "Wewe mheshimiwa, unawezaje kuhairisha kesi hii? Wakristo wana Krismasi, Pasaka, na sherehe zingine nyingi. Wayahudi wana Pasaka, Yom Kippur, na Hanukkah…alafu mteja wangu na wote wasioamini kwamba Mungu yupo hawana sikukuu kama hizo!" Hakimu aliinama kwenye kiti chake na akasema, "Ni wazi, kwamba mteja wako amechanganyikiwa hata asijue zaidi kusheherekea sikukuu yake ya wasioamini kwamba kuna Mungu!" Kwa kuropoka wakili akasema, "Mheshimiwa hatufahamu sikukuu hizo za waisoamini kwamba kuna Mungu. Mheshimiwa hiyo sikukuu itakuwa lini?" Hakimu akasema, "Inakuja kila mwaka katika tarehe kama hii – Aprili 1!

Maana kalenda yetu inaonyesha kwamba Aprili 1 ni siku ya wajinga", angalia kwamba Zaburi 14:1 na Zaburi 53 zinasema, "*Mpumbavu anasema moyoni mwake, kwamba hakuna Mungu…*". Hivyo basi, kwa mtazamo wangu, kama mteja wako anasema kwamba Mungu hayupo, basi kulingana na maandiko yeye ni mpumbavu, hivyo Aprili 1 ndio sikukuu yake!"

Mungu amechagua kuwachanganya wakatili katika hekima yao.

1 Kor. 1:27-29, "*Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; mwenye mwili awaye yote, asije akajisifu mbele za Mungu.*"

Bilashaka, tunawezza kuwa na hali ya uvumilivu itolewayo na maarifa na ujuzi…

Mara nyingi, unapojifunza zaidi, ndivyo unapogundua ni kiasi gani hujui. Na mara nyingi, kadiri unavyozeheka, ndivyo unavyotambua jinsi gani unafahamu kidogo.

Bila shak, tunaweza kuwa na hali ya uvumilivu kwa mfano wa Kristo, aliyekuwa tayari kutii mapenzi ya Baba yake.

- Yoh. 6:38, "*Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka.*"
- Yoh. 5:30, "*Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka.*"

Yesu hakufikiri zaidi yake binafsi kwamba aliona usawa na Mungu kama kitu kisichofaa kushikana nacho.

Fil. 2:6, "*Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho;*"

Tukiwa na nia ya Kristo tutaendelea mbele katika kusaidia kuwa na uvumilivu juu ya mtu binafsi.

Hitimisho

Huo ndio ubora wa "Nia Iliyofanywa Upya"…

- Nia inayofanana.
- Nia inayojishusha.
- Upole wa nia.

Kadiri tunavyoiga nia ya Kristo na kuifanya kuwa yetu…

- Ndivyo tutakavyofikiri sawasawa.
- Jinsi tutakavyo kuwa wangwana na waelekevu juu ya mambo mabaya
- Ndivyo tutakavyo shirikiana na wenye bahati kidogo
- Ndivyo tutakavyo kuwa wakengeufu na wakatili.

Hizo ndio sifa za wale walio na nia ya Kristo, na wanageuzwa kwa kufanywa upya nia zao.

Je tunaelekeza nia zetu kwenye mambo yalioko juu, Kristo aliko?

Kol. 3:1-2, "*Basi ikiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyojuu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.*"

Ikiwa tumefufuliwa pamoja na Kristo (kupitia ubatizo), hilo ndio jukumu letu!

Kol. 2:12, "*Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu.*"

Kama bado hatujafufuliwa na Kristo, kwa nini isiwe leo? Toa utii katika injili kwa imani, kutubu, kukiri, na kubatizwa ili uweze kuanza kutembea katika upya wa uzima!

- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Rum. 6:3-4, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo*

alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."